**MPANGO MKAKATI WA KUDHIBITI UVUVI HARAMU LINDI MC**

**UTANGULIZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ina mwambao wa bahari usiopungua wastani urefu wa km. 112 kutoka Mtaa wa Mkwaya kata Mingoyo hadi mtaa wa Likong'o kata ya Mbanja Kaskazini mwa Manispaa. Ukanda huu wa Bahari una fukwe nyingi zinazofaa kwa shughuli za uvuvi. Jamii ya wakazi waishio Mwambao zaidi hutegemea uvuvi katika Kujikimu kimaisha, Uvuvi wao hutumia zana/ teknolojia ya vyombo duni ambavyo huwalazimisha kuvua karibu na pwani. Vyombo hivyo ni ngalawa , mashua, madau, na mitumbwi .

**HALI YA UVUVI**

Hali ya ya uvuvi kwa Halmashauri ya Manispaa ni ya wastani kutokana na vyombo duni ambavyo vinatumiwa na wadau walio wengi visivyoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi, wengi wao hutegemea ngalawa na mitumbwi ambayo haitumii mashine ya kuwawezesha kufika mbali, hali hii inasababisha idadi kubwa ya wavuvi kuvua kandokando ya fukwe kwa kutumia muda mrefu bila kipato kinacholeta tija. hali hii duni inafanya baadhi ya wavuvi kuvua uvuvi haramu katika mwambao wa bahari na hata ndani ya bahari kwa kutumia milipuko na kokoro. Manispaa ya Lindi imeamua kushirikiana na ulinzi ushiriki ambao ni BMU's na wadau wengine wa uvuvi ili kutokomeza uvuvi haramu.

**Ufuatao ni mpango mkakati wa kudhibiti uvuvi haramu kwa kushirikiana na BMU**

| LENGO KUU (OBJECTIVES) | LENGO MAHUSUSI (Specific objective) | SHUGHULI (ACTIVITIES) | WAHUSIKA (STAKEHOLDERS) | MAHITAJI | GHARAMA (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutokomeza uvuvi haramu | Kutokomeza uvuvi haramu manispaa ya Lindi kwa kushirikiana na wadau wa uvuvi (BMU) | 1.Kutoa matangazo 50 kwa Wananchi na Wavuvi juu ya athari za uvuvi haramu na kuwataka wanaojihusisha na uvuvi haramu kujisalimisha wao wenyewe pamoja na zana za uvuvi haramu katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ndani ya siku 14 ifikapo juni 2017 | -Watendaji wa Kata/Mitaa, Polisi, BMU, Wataalamu wa uvuvi<br>-Waheshimiwa Madiwani | Kipaza Sauti, Gari, Mafuta na Vipeperushi | 300,000.00 |
| | | 2.Kuainisha mialo na makambi ya uvuvi yaliyopo Manispaa (landing site) | -BMU, Serikali ya Mtaa | -Shajala | 50,000.00 |
| | | 3.Kutoa elimu ya athari za uvuvi haramu kwa BMU 14 na vikundi 21 vya wavuvi ifikapok juni 2017 | -Afisa uvuvi, Serikali ya Mtaa, BMUs | -Gari na Mafuta | 300,000.00 |
| | | 4. Kufanya mikutano 20 ya ndani na nje kati ya BMU na Serikali za mitaa/kata ili | -Afisa uvuvi, Watendaji wa Kata/Mtaa, Wenyeviti | -Gari na Mafuta | 300,000.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuwatambua wavuvi haramu na kuwasilisha majina ya Wavuvi haramu kwa Mwenyekiti wa Kamati ya ulinzi na Usalamu ya Wilaya | wa Serikali ya Mtaa, Wadau wote wa uvuvi, Mhe, Diwani na Mh. Mkuu wa Wilaya | | |
| | | 5. Kufanya ukaguzi wa leseni za uvuvi, vyombo na usajili wa vyombo pamoja na zana zinazotumika kufanya shughuli za uvuvi. | -Afisa uvuvi, Watendaji Mtaa/Kata na BMU | Gari, Boti na Mafuta | 500,000.00 |
| | | 7. Kufanya ukaguzi wa samaki wanaoletwa sokoni/mwaloni ili kugundua kama ni wavuliwa kwa sumu au milipuko ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. | -Afisa uvuvi | | |
| | | 8. Kufanya doria 12 katika bahari kuu na pembezoni mwa bahari (pwani) na kuwachukulia hatua wale wote wanaokiuka sheria ya uvuvi ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009. | -Afisa uvuvi, BMUs, Watendaji wa Kata/Mtaa, Mwenyekiti wa Kamati ya ulinzi na usalama ya (KUU) Wilaya | Gari, Boti na Mafuta | 400,000.00 |
| | | 9. Kutoa zawadi kwa yeyote atakayefanikisha kukamatwa kwa wavuvi | | | 300,000.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | haramu.<br>10. Kutafsiri sheria ya uvuvi na kanuni zake kwa wananchi na wadau wa uvuvi ili zieleweke vizuri. | Mkurugenzi wa Manispaa<br>Afisa uvuvi | 50,000/= kwa tukio Shajala | 50,000.00 |

**JUMLA YA GHARAMA ZA UTEKELEZAJI: 2,200,000.00**

**MAJUKUMU YA BMU KATIKA KUTEKELEZA MPANGO KUDHIBTI UVUVI HARAMU**

1. Kuendeleza na kuhifadhi rasilimali za bahari kwa ajiri ya kizazi cha sasa na kijacho.

2. Kudhibiti na kutokomeza uvuvi haramu katika maeneo yao (vijiji, mialo, n.k)

3. Kuandaa mikutano kwa ajiri ya kutoa elimu juu ya athari zinazotokana na uvuvi haramu kwenye vijiji na mialo.

4. Kuandaa mkakati wa kutokomeza uvuvi haramu ngazi Mtaa

5. Kuhakikisha kuwa wavuvi wa eneo husika wanajisajiri kupitia kwenye ofisi za BMU ili kutambua idadi kamili ya wavuvi.

6.Kukagua makambi ya wavuvi, zana na leseni na kuwahamisisha wakate leseni kwenye mamulaka wanayotaka kufanya uvuvi (dago).

7. Kufanya doria za mara kwa mara kwenye maeneo yao ya kazi ili kuhakikisha wanatokomeza uvuvi haramu

8. Kuanisha majina ya watu wanaodhaniwa kuwa ni wavuvi haramu katika maeneo yao ya kazi.

**MAJUKUMU YA SERIKALI YA MTAA/KATA KATIKA KUTEKELEZA MPANGO KUDHIBTI UVUVI HARAMU**

1. Agenda ya uvuvi haramu iwe ya kudumu kwenye vikao vya ndani na mikutano ya hadhara.
2. Kushiriki na kusimamia doria katika maeneo yao ya kazi ili kutokomeza uvuvi haramu.
3. Kuandaa na kusimamia mikutano kwa ajiri ya kutoa elimu juu ya athari zinazotokana na uvuvi haramu kwenye vijiji na mialo.
4. Kuandaa mkakati wa kutokomeza uvuvi haramu katika ngazi za Mtaa/Kata
5. Kuendeleza, kusimamia na kuhifadhi rasilimali za bahari kwa ajiri ya kizazi cha sasa na kijacho.
6. Kusimamia usajiri wa wavuvi,wafanyabiashara wa mazao ya bahari, wakulima na wafugaji wa viumbe kwenye maji katika maeneo yao.
7. Kuhakikisha  wavuvi na wafanyabiashara wanasafirisha mazao ya bahari kuwa na vibali husika.

8. Kuhamasisha wavuvi haramu kusalimisha zana zao zilizokuwa zinatumika katika shughuli hizo.

**MAJUKUMU YA MAAFISA UVUVI KATIKA KUTEKELEZA MPANGO KUDHIBTI UVUVI HARAMU**

1. Kusajiri vyombo vya uvuvi/wavuvi
2. Kutoa leseni za uvuvi na vyombo vya uvivi
3. Kufanya doria
4. Kufanya sensa ya wavuvi na vyombo vya uvuvi
5. Kuainisha mialo (landing site) na makambi ya wavuvi
6. Kufanya ukaguzi wa mazao ya bahari yanayoletwa kwenye mialo/soko ili kutambua mazao yaliyovuliwa kwa uvuvi haramu
7. Kutoa elimu kwa wavuvi na wadau wote wa uvuvi athari za uvuvi haramu
8. Kutoa elimu ya ufugali wa viumbe kwenye maji
9. Kufanya mikutano mbalimbali kwa wavuvi, BMU na wadau wa uvuvi ya namna ya kulinda na kuhifadhi rasilimali za uvuvi
10. Kutembelea makambi ya wavuvi ili kukagua zana wanazokutumia kwenye shughuli za uvuvi na leseni zao.

**MAJUKUMU YA WAHESHIMIWA KATIKA KUTEKELEZA MPANGO KUDHIBTI UVUVI HARAMU**

1. Kuwezesha upatikanaji wa mahitaji yote muhimu yanayohitajika katika kutokomeza uvuvi haramu

**MAJUKUMU YA WAHESHIMIWA MADIWANI KATIKA KUTEKELEZA MPANGO KUDHIBTI UVUVI HARAMU**

1. Kuhakikisha agenda ya uvuvi haramu iwe ya kudumu kwenye vikao vya WDC na kwenye mikutano ya hadhara.

2. Kusimamia shughuli zote za kutokomeza uvuvi haramu.

**MAJUKUMU YA MKUU WA WILAYA KATIKA KUTEKELEZA MPANGO KUDHIBTI UVUVI HARAMU**

1. Kuhakikisha agenda ya uvuvi haramu inakuwa agenda ya kudumu katika vikao vya Kamati ya ulinzi na usalama (KUU) ya Wilaya
2. Kusimamia utekelezaji wa sheria ya uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 pamoja na kutoa maagizo juu ya uthibiti wa uvuvi haramu kwenye vyombo vya dola (Polisi nk)

**SHERIA YA UVUVI YA MWAKA 2003 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2009**

Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 pamaja na kanuni zake za mwaka 2009 kwa pamoja zimesisitiza mambo muhimu katika kuhakikisha rasilimali za bahari zinakuwa endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Ili kufanikisha hilo sheria inabainishaa kuwa;

1. Vyombo vyote vya uvuvi lazima visajiliwe na kupewa namba ya usajil ambayo itaandikwa ubavuni mwa chombo
2. Vyombo vyote vya uvuvi lazima viwe na leseni ya chombo
3. Wavuvi wote lazima wawe na leseni za uvuvi na wawe wamesajiliwa kwenye daftari la wavuvi
4. Nimarufuku kwa mtu yeyote kuvua kwa kutumia sumu, milipuko na kokoro
5. Ni kosa kuvua viumbe wa majini ambao wako hatarini kutoweka (endangered species) kama vile kasa (sea tuttle), makome (sea shells), jongoo bahari (sea cucumber) nguva (mermaids) kisukuku (silikanti) ambao wameanishwa kisheria
6. Ni kosa kusafirisha, kuingiza mazao ya bahari bila kuwa na kibali husika cha kukusanya na kusafirisha mazao ya bahari (Fishery movement permit).
7. Mtu yeyote haruhusiwi kuvuna mazao ya bahari katika maeneo yaliyotunzwa (marine protected areas) isipokuwa kwa kibali maalumu.
8. Ni kosa kwa yeyote kusafirisha na kuuza mazao ya bahari yatokanayo na uvuvi haramu.
9. Afisa uvuvi alieidhinishwa na serikali anatakiwa kukagua samaki wote wanaoletwa kwenye mialo na minada ya samaki ili kubaini kama wana sumu ama wanafaa kwa matumizi ya chakula.

10. Afisa uvuvi aliyeidhinishwa na serikali anatakiwa kuchukua tatwimu zote za uvuvi ikiwemo idadi ya samaki waliovuliwa, idadi ya vyombo vya uvuvi, zana zinazotumika kuvua samaki na idadi ya wavuvi kwa kushirikiana na BMU's.
11. Si ruhusa kwa mtu yeyote kusafirisha samaki wagonjwa (infected fish or fishery products) kutoka chanzo kimoja cha maji kwenda kingine ama kwa lengo kula
12. Si ruhusa kwa mtu yeyote kutengeneza, kuuza, kutunza, kumiliki ama kutumia ama kusababisha mtu mwingine kumiliki au kutumia kokoro kwenye miliki yeyote ya maji (bahari,ziwa, mto, bwawa).
13. Si ruhusa kwa mtu yeyote kutupa takataka kwenye chanzo/vyanzo vya maji ambazo zinasababisha uchafuzi wa mazingira
14. Uanzishwaji wa ufugaji wa viumbe maji utakuwa katika maeneo yote kama vile; baharini, mwambao wa bahari au bara kwa kibali afisa wa serikali aliyeidhinishwa na kwa kufuata taratibu zote utunzaji viumbe maji na mazingira yake, mfano si huhusa kukata mikoko kando ya bahari kwa kuwa ni mazalia ya samaki.

**ADHABU**

Mtu yeyote au kikundi cha watu watakao kiuka sheria tajwa hapo juu adhabu yake ni;

i) Kifungo kisichopungua miaka 7 kwa yeyote anayekutwa anavua samaki kwa kutumia sumu.

ii) Kifungo kisichopungua miaka 5 kwa yeyote atakayekutwa anavua samaki kwa kutumia milipuko

iii) Kifungo kisichopungua miaka 3 gerezani kwa yeyote atakayekutwa anavua kwa kutumia kokoro pamoja na makosa mengine tajwa hapo juu

iv) Au kufungwa pamoja na kulipa faini ya Shilingi 100,000/= hadi 1,000,000/= kutegemea na kosa lililofanyika.